# CHUO CHA AFYA BLUE PHARMA

P.O. Box 1570, Singida, Tanzania,
Website: www. bphacoh.ac.tz
*Email: info@bphacoh.ac.tz, Tel: +255743358048*

---

**12 Oktoba 2025**

**Kumb. Na. BPCH/SGD/B/14/30**

**Kwa:** Wanafunzi wote

**YAH: TANGAZO LA MATOKEO YA AWALI YA MITIHANI YA KUMALIZA MUHULA WA 2 WA MWAKA WA MASOMO 2024/2025 NA MAELEKEZO MENGINE**

1. Kwa tangazo hili ninawataarifu wanafunzi kuwa matokeo ya awali ya mitihani ya kumaliza muhula wa 2 wa mwaka wa masomo 2024/2025 yametolewa rasmi na barua ya Wizara ya Afya yenye kumbukumbu namba: CLB.71/262/01/83 ya tarehe: 7 Oktoba 2025. Matokeo haya yanapatikana katika akaunti ya mwanafunzi ya mfumo wa Kumeneji rekodi za mwanafunzi kupitia kiungo https://srmis.bphacoh.ac.tz .
2. Ufafanuzi wa matokeo husika ni kama ifuatavyo:
   a. Mwanafunzi aliyepata hali ya matokeo (Status/Remark) ya **First, Second, Upper Second, Lower Second,** na **Pass** katika matokeo yake, amefaulu mitihani kikamilifu na anasifa ya kuendelea na masomo ya muhula wa kwanza wa mwaka wa masomo 2025/2026 utakaoanza rasmi tarehe **3 Novemba 2025.**
   b. Mwanafunzi ambaye amepata hali ya matokeo (Status/Remark) ya **Supp**, anatakiwa kufanya mtihani wa marudio kwa baadhi ya masomo ambayo hakuyafaulu katika mtihani wa kumaliza muhula wa 2 ya awamu ya kwanza. Mitihani ya marudio (Supplementary) ya muhula wa pili, 2024/2025 inategemewa kuanza kufanyika katika tarehe zitakazoelekezwa hapo baadae. Aidha, Mwanafunzi huyu kwa utashi wake mwenyewe, anaweza kuendelea na masomo ya muhula wa 1 wa mwaka wa masomo 2025/2026 huku akijiandaa na mitihani ya marudio kwa masomo husika.

BLUE PHARMA COLLEGE OF HEALTH
PRINCIPAL (BPHACOH) P.O. Box 1570
★ SINGIDA ★

c. Mwanafunzi ambaye amewekewa "**W**" kwenye matokeo yake maana yake ni kuwa amefichiwa matokeo kutokana na kutokamilisha malipo ya ada ya muhula wa 2, 2024/2025. Mwanafunzi huyu ataona matokeo yake baada ya kukamilisha malipo husika na kupata uthibitisho wa kimaandishi wa Mhasibu wa Chuo kuwa malipo husika yamepokelewa.

d. Mwanafunzi ambaye amepata hali ya matokeo (Status/Remark) ya **Fail,** ameshindwa kufikisha GPA ya 2.0 hatoruhusiwa kuendelea na masomo ya muhula wa 1, 2025/2026. Hata hivyo, mwanafunzi huyu anaweza kusajiliwa (re -admitted) tena katika muhula wa 2 wa mwaka wa masomo 2025/2026 utakaoanza mwezi Aprili 2026 kwa ajili ya kusoma upya masomo ya muhula huo.

e. Mwanafunzi ambaye amepata hali ya matokeo (Status/Remark) ya **Repeat Module** maana yake ni kuwa amefeli (Amepata alama chini ya 50%) kwenye zaidi ya nusu ya mitihani ya mwisho (semester examination) ya masomo yaliyotahiniwa katika muhula pili, 2024/2025. Mwanafunzi huyu atatakiwa kuwasili katika muhula wa 2 utakaoanza mwezi Aprili 2026 ili kusoma upya masomo husika aliyoyafeli.

3. Dirisha la kuwasilisha rufaa dhidi ya matokeo ya kumaliza muhula wa 2, 2024/2025 liko wazi kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe **20 Oktoba 2025.** Mwanafunzi ambaye atakata rufaa dhidi ya matokeo husika, atatakiwa kuandika barua kwenda kwa ofisi ya Mkuu wa Chuo huku akiainisha somo/masomo ambayo matokeo yake anayakatia rufaa na sababu za kukata rufaa. Gharama ya kukata rufaa ya matokeo kwa somo moja ni **shilingi za kitanzania elfu hamsini (50,000/=),** itakayolipwa baada ya rufaa husika kupitishwa na kamati ya taaluma ya chuo.

4. Kila mwanafunzi mwenye sifa ya kuendelea na masomo ya muhula wa 2, 2024/2025 atatakiwa kulipa kiasi cha Shilingi za kitanzania **605,000/=,** walau kiasi cha ada ya awamu ya kwanza ya malipo (**Tzs. 400,0000/=**) na kiasi cha malipo ya bweni kwa muhula wa kwanza (**Tzs. 200,000/=**) Kwa wanafunzi wa bweni ili aweze kupokelewa na kusajiliwa kuendelea na masomo ya muhula wa 1, 2025/2026.

5. Mwanafunzi mwenye hali ya kimatokeo ya **Supp** na anaridhia kuendelea na masomo ya muhula wa 1, 2025/2026 huku akijiandaa na kusubiri kufanya mitihani ya marudio ya mwaka 2024/2025 itakayoanza tarehe **27 Novemba 2025,** atalipa kulingana na makubaliano maalumu atakayosaini na ofisi ya Mkuu wa Chuo. Aidha, masomo ya jioni (remedial classes)



BLUE PHARMA COLLEGE OF HEALTH
PRINCIPAL
(BPHACOH)
P. O. Box 1570
SINGIDA

kwa wanafunzi wenye supp na watakaoridhia kuendelea na masomo ya ngazi inayofuata yataanza mara moja tarehe **3 Novemba 2025.**

6. Kutakuwepo na paneli maalumu ya kupokea na kusajili wanafunzi kwa ajili ya masomo ya muhula wa 1, 2024/2026. Paneli itafanya kazi hiyo siku ya Jumamosi ya tarehe **1 Novemba 2025** na Jumapili ya tarehe **2 Novemba 2025.** Hivyo ni jukumu la kila mwanafunzi kupitia kwenye paneli husika kabla ya kuingia darasani kuendelea na masomo. Ofisi ya Mkuu wa Chuo **hakitahusika** na changamoto za kiusajili zitakazojitokeza kwa mwanafunzi ambaye hatopita kwenye paneli hiyo.
7. Nawatakia utekelezaji mwema.

G.M. Laurian

Kny: Mkuu wa Chuo

BLUE PHARMA COLLEGE OF HEALTH
PRINCIPAL
(BPHACOH)
P. O. Box 1570
SINGIDA

---

**Nakala kwa:**

1. Ubao wa Matangazo; na
2. Tovuti ya Chuo